UTEKELEZAJI WA DIRA YA TAIFA YA MWAKA 2025:KANDA YA ZIWA

1. Utangulizi

Toleo hili la Darubini ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 linaelezea utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Mikoa hiyo ni Mwanza, Kagera, Geita, Simiyu, Marana Shinyanga.Toleo hili litaonesha ni kwa kiasi gani Serikali imetekeleza nguzo zote za Dira 2025 katika Kanda hii. Nguzo hizo ni: (i) Kuboresha hali ya maisha ya Watanzania; (ii) Kuwepo kwa mazingira ya amani,utulivu na umoja; (iii) Kujenga utawala bora na utawala wa sheria; na (iv) Kujenga uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani kutoka nchi nyingine.

2. Utekelezaji wa nguzo za Dira 2025

Pamoja na kuelezea hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kutekeleza nguzo za Dira 2025 katika Kanda ya Ziwa, sehemu hii inaelezea mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizopo.

2.1 Utekelezaji wa nguzo ya kwanza ya Dira 2025

Nguzo ya kwanza ya Dira 2025 iliweka malengo yafuatayo: Kuwa ifikapo mwaka 2025 Tanzania: (i) iwe na usalama wa chakula; (ii) itoe elimu ya msingi kwa watoto wote; (iii) uwepo usawa wa kijinsia kwenye masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa; (iv) iwe na huduma bora za afya kwa wananchi wote; (v) itoe huduma bora za afya ya uzazi kwa rika mbalimbali; (vi) ipunguze vifo vya watoto wachanga na vifo vya wanawakevitokanavyo na uzazi; (vii) kuwepo na maji safi na salama; (viii) wastani wa umri wa kuishi uongezeke kufikia kiwango cha nchi za kipato cha kati; na (ix) iondokane na umaskini uliokithiri. Sehemu hii itaeleza jinsi gani Serikali imetekeleza malengo hayo katika Kanda ya Ziwa na changamoto zilizopo.

Katika kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula, Serikali ya Tanzania imekuwa ikigharamia miradimbalimbali ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini ili kukuza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuwawezesha wananchi wote kumudu bei za vyakula.Miradi hiyo inatekelezwa kupitia Programu ya Kukuza Maendeleo katika Sekta ya Kilimo nchini (ASDP1), Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani (NIMP2),Mpango wa Kuendeleza Kilimo cha UmwagiliajiMaji Mashambani katika Mwambao wa Ziwa Viktoria, Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya (DADPs3),Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (PIDP4) na miradi mingine ya maendeleo ya kilimo kwa kushirikiana na wafadhili wa nchi mbalimbali.Baadhi ya skimu na mabwawa ya umwagiliaji yaliyojengwa na kukarabatiwa chini ya programu hizo katika mikoa iliyopo Kanda ya Ziwa kuanzia mwaka 2000 hadi 2013 yameainishwa katika jedwali lifuatalo:

Skimu na Mabwawa ya Umwagiliaji Yaliyojengwa na Kukarabatiwa

Mkoa	Mabwawa ya umwagiliaji yaliyojengwa	Skimu zilizojengwa/kukarabatiwa
Mwanza	Miyogwezi (Ukerewe); Luhala (Kwimba); Sukuma (Sengerema)	Igongwa (Misungwi); Ukerewe (hekta 200); Kalemela-Magu (hekta 20); Mbarika-Misungwi (hekta 45); Luchili (hekta 500); Nakatunguru (hekta 20); Kimiza; Luhala; Shilanoma; Katuguru-Sengerema (hekta 400); Sawenge na Chabura-Magu; Nyambeho, Misungwi (hekta 180); Kimiza Kwimba (hekta 153); Shilanona, Kwimba (hekta 201);Igenge (Misungwi)
Kagera	Nkenge-Bukoba (hekta 40) Nyaishozi, Karagwe (hekta 50)	Nkenge-Bukoba (hekta 500); Bugorora-Bukoba (hekta 100); Bigombo (Ngara); Kyakakera (Missenyi); Kyamyorwa (Muleba); Mwiruzi (Biharamulo)
Shinyanga	Isholo, Bukombe na Mangwila;	Nyida, Shinyanga (hekta 289); Itilima, Shinyanga (hekta 225); Masengwa, Shinyanga (hekta 337); Itilima; Bubale/Masegwa; Malampaka;Bukigi, Maswa (hekta 150); Mwagwila (Meatu); Kinamwigulu (Maswa)
Mara	Nyamitita(Serengeti);Rabuor (Rorya); Kisangwa (hekta 650); Mesaga (hekta 170); Maneke (hekta 200); Masinono (Butiama), Kisangwa (Bunda);	Buswahili (Musoma), Balili (Bunda), Ochuna -Tarime(hekta 300) Bwanza (hekta 20) na Tamau (hekta 20); Kahangara (hekta 20); Mkoma (hekta 20); Nyabangu (hekta 20), Chanyauru (hekta 20); Nyatwali (hekta 20) Butiama-Musoma (hekta 320); Suguti-Musoma hekta 2,000); Namhula; Bugelela-Serengeti; Kahanga (Kahama)
Geita		Lwenge (Geita); Nampangwe (Bukombe), Nyisanzi (Chato)
Simiyu	Nampangwe	Lutubiga (Busega); Mwasubuya (Bariadi)

Matumizi ya mabwawana skimu za umwagiliaji yameongeza eneo la ardhi ya kilimo cha umwagiliaji, ambapo katika mkoa wa Shinyanga eneo la umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 3,785 mwaka 2002 hadi kufikia zaidi ya hekta 30,000 mwaka 2009. Vilevile Mkoani Mwanza, kilimo cha umwagiliaji kimeongezeka kutoka hekta 1,173 mwaka 2005 hadi hekta 3,532 mwaka 2010.

Takwimu za Wizara ya Kilimo na Ushirika zinaonyesha kuwa kilimo cha umwagiliaji kimechangia ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula kama vile mahindi, mpunga, mihogo, mtama na viazi vitamu kutoka tani 316,187 mwaka 2002 hadi tani 686,066 mwaka 2013 katika mkoa wa Shinyanga.Vilevile katika mkoa wa Mwanza,uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula umeongezeka kutoka tani 685,642 mwaka 2005 hadi tani 968,654 mwaka 2010; sawa na ongezeko la asilimia 41. Mafanikio haya katika sekta ya kilimo yamechangiwa pia na chuo kikubwa cha utafiti wa kilimo cha Kanda kilichopo Ukiriguru ambako kinazalisha mbegu bora za mazao ya chakula na biashara.

Pia, Wizara kupitia Vituo vya Utafiti vya Uyole, Mlingano na Selian ilisambaza teknolojia ya Kilimo Hifadhi katika Kanda ya Ziwa, kupitia Halmashauri za wilaya za Bukoba, Bunda, Magu, Serengeti, Meatu, Maswa, Sengerema na Geita, ambapo wakulima huzingatia kanuni za kilimo hifadhi. Hii imepelekea ongezeko la tija katika zao la mahindi kutoka magunia 3 mwaka 2005 hadi wastani wa magunia 20 kwa ekari katika mwaka 2013.

Katika kutekeleza Dira 2025, Serikali imeendelea kuhakikisha elimu ya msingi inatolewa kwa watoto wote, ambapo mwaka 2000, Serikali iliondoa ada katika shule za msingi za Serikali ili kila mtoto aweze kupata elimu ya msingi. Mafanikio yameonekana zaidi katika mkoa wa Shinyanga ambapo kwani takwimu za Wizara ya Elimu zinaonesha kumekuwa na ongezeko la idadiya watoto wenye umri kati ya miaka 7 hadi 13 wanaosoma katika shule za msingi,kutoka asilimia 83.9 mwaka 2003 hadi kufikia asilimia 92.9 mwaka 2013. Katika mikoa wa Mara, Kagera na Mwanza idadi imepungua. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na tatizo la utoro wa wanafunzi na baadhi ya wazazi kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa elimu kwa mtoto.



Changamoto kubwailiyopo ni kiwango duni cha elimu inayotolewa katika ngazi zote za elimu, kutokana na upungufu wa walimu, nyumba za walimu, madarasa, vitabu pamoja na vifaa vingine vya kufundishia. Kwa mfano, katika mkoa wa Mwanza, hadi kufikia mwaka 2010 kulikuwa na upungufu wa madarasa 10,820, sawa na asilimia 54; na upungufu wa nyumba za walimu 16,271, sawa na asilimia 85.Hali hii inakwamisha maendeleo ya elimu kwa watoto, na ya taifa kwa ujumla. Aidha, inachangia pia kupanuka kwa pengokatiya matajiri na maskini nchini.

Kwa kutambua umuhimu wa usawa wa kijinsia katika kuchochea maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, pamoja na Wizara ya Elimu zimekuwa zikifanya jitihada mbalimbali za kuleta usawa wa kijinsia nchini. Katika mwaka 2011, Serikali ilizindua harambee ya ujenzi wa mabweni 30 ya wasichana katika shule za Halmashauri za Wilaya 8, ambapo katika kanda ya Ziwa, Wilaya za Geita na Musoma zitapata fedha kwa ajili ya ujenzi huo.

Afya bora ni nguzo na raslimali muhimu katika kuchangia maendeleo nchini, hususan katika kuboresha hali yamaisha na kupunguza umaskini. Kwa mantiki hii Serikali imeongeza ujenzi wa hospitali, zahanati na vituo vya afya katika mikoa iliyopo katika kanda ya Ziwa; lengo likiwa ni kurahisisha na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote. Taarifa za Ofisi ya Takwimu ya Taifa zinaonesha ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya katika Kanda ya Ziwa kama inavyooneshwa kwenye mchoro ufuatao:



Ongezeko hili la vituo ya kutolea huduma za afya limechangia kupunguza vifo vya watoto katika kanda ya Ziwa kama inavyooneshwa kwenye mchoro ufuatao:



Changamoto iliyopo katika sekta ya afya kwenye Kanda ya Ziwa, ni uwepo wa vituo vingi vya huduma za afya ambavyo vyote vinahudumiwa na ghala moja tu la dawa, ambalo halitoshelezi mahitaji ya dawa na vifaa tiba. Kwa sababu hiyo, kuna upungufu mkubwa wa vifaa, na madawa yanayohitajika kukidhi mahitaji halisi ya wagonjwa.

Katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama,Serikali imekuwa ikiboresha huduma za maji mijini na vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji ya kitaifa. Katika Kanda ya Ziwa, miradi mikubwa ya kitaifa ni pamoja na mradi wa kutoa maji toka Ziwa Victoria kwa ajili ya matumizi ya wananchi wapatao 450,000 katika miji ya Kahama na Shinyanga. Mpango uliopo ni kupanua mradi huo ili kuwafikia watu wapatao milioni moja ifikapo mwaka 2025. Mradi wa Maji wa Mgango/Kiabakari/Butiamauna uwezo wa kuwapatia maji zaidi ya wananchi 60,000 katika vijiji 13. Pia, Serikali imeanzisha Mradi wa maji wa Maswa mkoani Shinyanga unaohudumia wakazi wa mji wa Maswa pamoja na vijiji vya Zanzuli, Malita, Buyubi, Dodoma, Hinduki, Mwadila, Mwabayanda na Mwasita.Miradi mingine ya maji safi iliyoanzishwa ni Wegero (Musoma), Mwanjoro (Meatu), Seke Ididi (Kishapu), Habiya (Bariadi), Bundaza (Missenyi), Rulenge (Ngara) na mradi wa maji wa Geita wenye uwezo wa kuhudumia wakazi 68,500.

Changamoto kubwa iliyopo kwenye usimamizi wa rasilimali za maji ni kupungua na kuharibika kwa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za kibinadamu. Changamoto nyingineyo ni ongezeko la idadi ya watu katika miji mikubwa,ikilinganishwa na rasimali za upanuzi wa huduma za maji mijini.Miundombinu ya maji iliyojengwa haitoshelezi mahitaji ya idadi ya watu waliopo, mfano katika miji ya Ngudu, Magu, Geita na Ukerewe,

[1] *Agricultural Sector Development Programme*
[2] *National Irrigation Master Plan*
[3] *District Agricultural Development Programmes*
[4] *Participatory Irrigation Development Programme*

katika mkoa wa Mwanza.

Ili kuondoa umaskini uliokithiri kwa wananchi,hususan waliopo vijijini, jitihada zilizofanywa na Serikalini pamoja na kuanzishwa kwa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN5) unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF6 kuanzia mwaka 2000, kwa kushirikiana naBenki ya Dunia. Katika kanda ya Ziwa, mpango huo umekuwa ukitekelezwa wilayani Bunda (Mara), ambapo wananchi 1,269 katika vijiji 20 wamenufaika.

2.2 Utekelezaji wa nguzo ya pili ya Dira 2025

Nguzo ya pili ya Dira 2025 inalenga kuimarisha amani, utulivu na umoja wa nchi ili kustawisha maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Sehemu hii itaeleza jinsi gani Serikali imetekeleza malengo hayo katika Kanda ya Ziwa na changamoto zilizopo. Pamoja na kwamba ni jukumu la kila Mtanzania na kila raia mwema kushiriki kikamilifu kulinda amani na utulivu wa nchi, Serikali imekuwa ikiongoza jitihada hizo kwa kutumia Majeshi ya Ulinzi na Usalama, kupitia operesheni mbalimbali, kukamata wahalifu na kuwashitaki kwa mujibu wa sheria. Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kukabiliana na tatizo la uhamiaji haramu nchini kupitia operesheni maalumu iliyopewa jina la 'Operesheni Kimbunga', kwa lengo la kuwaondoa nchini watu wote ambao hawana uraia au haki ya kisheria kuishi nchini. Katika mikoa iliyopo Kanda ya Ziwa, Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji wamefanikiwa kukamata wahamiaji haramu 209 mkoani Kagera na 50 mkoani Geita, kutoka nchi za Burundi, Rwanda, Congo na Uganda. Pamoja na juhudi hizo, katika kanda ya Ziwa kumekuwa na matukio mengi yauvunjifu wa amani, kama vile mauaji ya albino na vikongwe, yaliyochochewa kwa kiasi kikubwa na imani za kishirikina Jeshi la Polisi linaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa wahusika wote wa matukio hayo ya uvunjifu wa amani wanakamatwa na kufikishwa mahakamani, ili wahukumiwe kulingana na sheria za nchi.

2.3 Utekelezaji wa nguzo ya tatu ya Dira 2025

Nguzo ya tatu ya Dira 2025inalenga katika kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria kwa kujenga jamii yenye sifa zifuatazo (i) maadili mema na kuthamini utamaduni; (ii) uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria; (iii) isiyokuwa na rushwa na maovu mengine; na (iv) iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine, na yenye kumiliki na kubaini ajenda za maendeleo.

Ili kujenga uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria, mnamo mwaka 2007, Serikali ilianzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili kuondoa athari za rushwa katika maendeleo ya jamii kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Taasisi hiyo imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali ili kubaini mianya ya rushwa na kuweka mikakati ya kuitokomeza. Kwa mfano, katika mkoa wa Shinyanga TAKUKURU kwa kushirikiana na viongozi wa Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe iliweka mikakati wa kudhibiti mianya ya rushwa katika uvunaji wa mazao ya misitu.

Serikali pia imekuwa ikifanya jitihada za kujenga jamii iliyoelimika na inayojiamini, ambapo mwaka 2014 Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa mara ya kwanza ilianzisha maadhimisho ya Wiki ya Elimu nchini. Lengo la maadhimisho hayo ni kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kila mwananchi kuchangia katika kuchochea ari ya kuwa na elimu bora. Jedwali lifuatalo linaonyesha idadi ya shule zilizopata tuzo kwa ufaulu mzuri katika kanda ya Ziwa:

Shule Zilizopata Tuzo kwa Ufaulu Mzuri katika Kanda ya Ziwa

Mkoa	Shule za Msingi	Shule za Sekondari	Jumla
Geita	5	1	6
Kagera	320	11	331
Mara	165	7	172
Mwanza	224	20	244
Shinyanga	61	11	72
Simiyu	2	3	5

[5] *Productive Social Safety Net*
[6] *Tanzania Social Action Fund*

2.4 Utekelezaji wa nguzo ya nne ya Dira 2025

Nguzo ya nne ya Dira 2025 inalenga katika kujenga uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani kutoka nchi nyingine. Lengo hilo limepangwa kutimizwa kwa kujenga sekta shindani ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ili kujenga uchumi endelevu na kufikia maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha kati, ifikapo mwaka 2025. Moja ya Wizara zinazohusika katika kutekeleza nguzo hii ni Wizara ya Ujenzi, kupitia miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja, ili kufungua fursa za maendeleo katika maeneo malimbali ya nchi ilikurahisisha usafirishaji na upatikanaji wa bidhaa na huduma. Katika mikoa iliyopo Kanda ya Ziwa, Serikali imefanikisha ujenzi wa barabara zifuatazo kwa kiwango cha lami:

Barabara Zilizojengwa kwa Kiwango cha Lami Kanda ya Ziwa

	Barabara	Urefu wa barabara (kilometa)	Mwaka wa ujenzi hadi kukamilika
Mwanza	Sengerema - Usagara	40 km	2008 - 2010
	PMMR Mwanza Mashariki	208.4 km	2007 - 2013
Geita	Geita - Usagara	90 km	2008 - 2010
	Buzirayombo - Geita	100 km	2005 - 2008
	Kyamyorwa - Geita	220 km	2008
	Kyamyorwa - Buzirayombo	100 km	2005 - 2008
Kagera	Uyovu - Bwanga - Biharamulo	112 km	2012
	Kyaka - Bugene	59.1 km	2013
	Lusahunga - Isaka	382 km	2010 - 2013
	Lusahunga - Rusumo - Kobero/Nyakasanza	150 km	2013 - (Unaendelea)
	Mutukula - Bukoba - Biharamulo - Lusahunga	294 km	2009 - 2013
Shinyanga	Isaka - Ushirombo	132 km	2009 - 2013
	Ushirombo - Lusahunga	110 km	2010 - 2013
	Shinyanga - Mwigumbi - Maswa - Bariadi	171 km	2013 - (Unaendelea)
Mara	Nyanguge - Musoma	183 km	2010 - 2013
Simiyu	Simiyu/Mara (mpakani) - Musoma	85.5 km	2010 - 2013

Serikali pia imefanya jitihada kuongeza viwanda kwa ajili ya kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania na kuuzwa nje ya nchi. Jitihada hizo ni pamoja na uanzishwaji Mamlakaya Kusimamia Maeneo Huru ya Uzalishaji (EPZA7) mnamo mwaka 2006 ambapo ndani ya maeneo hayo miundombinu iliyoboreshwa na vivutio hutolewa kwa wawekezaji, lengo likiwa ni kukuza uwekezaji ambao utalenga kuimarisha uuzaji bidhaa nje ya nchi na kuongeza mapato ya nchi. Katika Kanda ya Ziwa, maeneo huru ya uzalishaji yametengwa katika eneo la Kitengule (Mwanza) na Bukoba (Kagera). Vilevile, Wizara ya Viwanda na Biashara imehamasisha usajili wa biashara, ambapo biashara zaidi ya 50 katika mipaka ya Sirari na Shirati (Mara) na Mtukula (Kagera) zimepewa elimu na kusajiliwa kwa lengo la kuziwezesha kuuza bidhaa katika nchi zote za Afrika Mashariki.

Economic and Social Research Foundation (ESRF)
P.O. Box 31226, Dar es Salaam, Tanzania.
Phone: (+255) 754 780 133, (+255) 777 790 133,
(+255) 782 780 133 • Fax: (+255 22) 2760062
E-mail: esrf@esrf.or.tz • Website: www.esrf.or.tz

[7] *Export Processing Zones Authority*

DARUBINI YA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025

TOLEO LA KANDA YA ZIWA

Toleo la **SITA**

ESRF